HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA.

OFISI YA AFISA MTENDAJI
KATA YA MWASANGA,
S.L.P. 149,
MBEYA.
9 - 5 - 2007.

THE FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY
HAIDERY PLAZA, GHOROFA YA 5,
MTAA WA UPANGA / KISUTU
S.L.P. 7192
DAR-ES-SALAAM.

YAH:-

KINYANG'ANYIRO CHA ASASI BORA YA UDF

Kutokana na mafunzo ya siku tano yaliyofanyika na UDF asasi isiyo kuwa ya kiserikali katika kata zote nne kata ya mwasanga, mwakibete Tembela, na Ikomba juu ya kuelimisha Jamii kujua haki zao na wajibu wao (utawala bora)

Baada ya mafunzo hayo sisi katika kata ya mwasanga tuliibuka na mawazo yafuatayo:-

(a) ujenzi wa sekondari katika eneo letu tumepanga wananchi wafyatue matofali 30,000; Tutaanza kufyatua matofali mwezi wa saba 2007.

(b) ujenzi wa zahanati ya kata hii tutaanza kushughulikia mwezi wa nane 2008.

(c) Utengenezaji wa Barabara za mitaa kwa kutumia nguvu za wananchi

(d) ujenzi wa daraja kutoka mtaa wa Nduguya kwenda mtaa wa Isoso hadi tarafa ya Igale Wilaya ya mbeya vijijini.

Hili tunaomba serikali itusaidie mwakani Daraja liwe limejengwa. Wananchi tupo tayari kuchangia nguvu zetu.

Mambo hayo yote ~~yatikuwa~~ yaliibuka kwenye mafunzo ya utawala bora na tumekaa vikao na wananchi wetu, baada ya mafunzo hayo na yamepitishwa.

Tunaomba hii ASASI ingie kwenye kinyang'anyiro hicho kwa uwazi na uwajibikaji wao katika mafunzo hayo.

Nakutakia kazi njema

[signature]

V. M. MPOLI
AFISA MTENDAJI KATA

KWA BAHATI MBAYA MUHURI ULIFUNGIWA KWENYE DRAW NI MATUMAINI YA AFISI KUWA UTAIPOKEA TAARIFA HII.